

**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI  
HALMASHAURI YA MJI BARIADI  
SHULE YA SEKONDARI SIMIYU**

S.L.P 301,  
**BARIADI.**

TAREHE ...../...../.....

**MAWASILIANO - SIMU: 0764/0784-481046/0622563754/0753976753**

Kumb Na. **SSS/JI/2021/....**

**Jina la Mwanafunzi.....**

S.L.P.....

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SIMIYU ILIYOPO  
MJI WA BARIADI, MKOA WA SIMIYU MWAKA 2021**

## **1. UTANGULIZI**

Ninafurahi kukuarifu kwamba **umechaguliwa** kujiunga na kidato **KWANZA** katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari **SIMIYU** ipo umbali wa km 2.36 Mashariki mwa Halmashauri ya Mji wa Bariadi unapita barabara ya NMB Bariadi. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia **tarehe 11/01/2021** kwa ajili ya usajili na maelekezo ya taratibu za shule na masomo kuanza na mwisho wa kuripoti ni tarehe **28/01/2021** (ndani ya siku 14 za masomo) ambapo taarifa itatolewa kwa wasioripoti ili kufanyika kwa chaguo la pili.

## **2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

### **2.1. Sare za Shule**

- ✓ Sare ya shule hii ni **SURUALI** mbili kwa Wavulana na **SKETI** mbili kwa Wasichana
- ✓ Rangi ya **vitambaa** imeambatanishwa kwenye fomu na utapewa ushauri kuhusu mshono wakati wa kuchukua fomu.
- ✓ Hijab inaruhusiwa kwa ndugu Waislam, ila rangi ya **hijab** ifanane na sare ya shule (mshono utaelekezwa).
- ✓ Shati au Blauzi ziwe rangi nyeupe na mikono mifupi.
- ✓ Viatu **vyeusi** vya ngozi jozi 2 vyenye kamba (**gidamu**) na kiwe na kisigino kifupi. Viatu aina ya **RABA** haviruhusiwi kuvaliwa kama sare ya shule isipokuwa wakati wa michezo tu.
- ✓ Soksi **nyeupe ndefu** jozi 2 kwa wavulana na wasichana na sivinginevyo.
- ✓ Mkanda wa suruali uwe wa ngozi, na uwe na belt ndogo.
- ✓ Vifaa vya michezo, bukta, viatu na fulana za mazoezi zitatolewa maelekezo wakati wa kuchukua fomu.
- ✓ Mwanafunzi atatakiwa kuwa na **SWETA** rangi ya **kijani** kwa ajili ya kujikinga na baridi.

## **2.2. Vifaa vya Kujifunzia**

- ❖ Daftari kubwa 12 aina ya Counterbooks
- ❖ Dictionary (kamus) ya kiingereza (English – English translation)
- ❖ Mathematical set (mkebe wa hisabati) 01
- ❖ Kalamu za wino blue/nyeusi na kalamu za risasi za kutosha.

## **2.3 Vitu vyote vitakaguliwa wakati wa usajili.**

- Pamoja na barua hii zimefungashwa fomu ambazo zitajazwa kikamilifu kabla ya kuzikabidhi kwa MSAJILI wa mwanafunzi.
- **Medical examination form** ambayo itajazwa na na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
- Fomu ya taarifa muhimu za Mwanafunzi iiazwe kwa ushirikiano na Mzazi/Mlezi
- Kwa yule tu aliye na **matatizo ya kiafya** aje na cheti cha **DAKTARI** kwa uthibitisho ili atambulike shuleni.
- Sheria, Taratibu na Kanuni zote za shule zimeambatanishwa, mzazi/mlezi pamoja na mwanafunzi mwenyewe kama mhusika zisomwe kwa umakini na kuzifahamu maana ndio mwongozo wa mwanafunzi akiwa shuleni.

**Karibu Sana  
Shule ya Sekondari Simiyu**

.....  
**PAUL R. SUSU  
MKUU WA SHULE**